# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO YA WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI KWA MWAKA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaaliwa uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa ambao ni wa mwisho katika Baraza la Kumi la Wawakilishi Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia Kanuni ya 103 (6) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2024, natumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati inaendelea kupongeza juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi wa Dr. Hussein Ali Mwinyi anaeendelea kudhihirisha maono mapana ya kimaendeleo yanayolenga upatikanaji wa huduma bora za kijamii kwa kila mwananchi. Katika kipindi hiki cha uongozi wa Rais Mwinyi tunaendelea kushuhudia miradi mingi ya uimarishwaji wa Miundombinu ya nishati ya

maji na umeme ambazo ni rasilimali muhimu sana katika jamii, pamoja na kudhibiti uvunaji holela wa rasilimali zisizorejesheka ili kulinda taswira na haiba nzuri ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Utangulizi huo sasa niko tayari kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu utekelezaji wa Wizari ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Bajeti kwa Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## UKUSANYAJI WA MAPATO

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa kipindi cha robo tatu ya utekelezaji wa Bajeti ni asilimia **111%** ya lengo la Makadirio ya Mwaka. Kiwango hiki cha ukusanyaji wa Mapato ni dalili nzuri kwa Wizara kuvuka lengo la ukusanyaji kwa mwaka huu yanayotokana na kianzio chake cha uvunaji wa Rasilimali zisizorejesheka. Vile vile, hali hiyo inaonesha kwamba upangaji wa malengo haya ya ukusanyaji ulizingatia uhalisia wa mwenendo wa ukusanyaji wa ada ya mchanga, mawe na kokokoto.

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA

### Vipaumbele vya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imechambua utekelezaji wa Programu za Wizara ya Maji, Nishati na Madini zinazotokana na Vipaumbele sita (6) walivyojiwekea kwa mwaka 2024/25 ambavyo kimsingi ni sawa na Vipaumbele vitano (5) walivyojiwekea kwa Mwaka ujao wa Fedha kama vinavyoonekana kwa kina katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na utekezaji mzuri wa vipaumbele hivyo, Kamati inawaomba watendaji wa Wizara hii kuongeza bidii ya uwajibikaji ili kuongeza ufanisi katika upatinaji wa huduma za kijamii hasa Maji safi na Umeme ili kupunguza kero za wananchi zinazosababishwa na ukosefu na uhafifu wa huduma hizo katika sehemu kadhaa tunazoishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa hakika, sote hapa ni mashahidi kwani tunapozunguka katika maeneo yetu ama kupitia katika vyombo vyetu vya habari, kilio kikubwa cha wananchi ni ukosefu wa huduma ya maji safi ikiwa haiwafikii kabisa au utokaji wake sio wa kuridhisha pamoja na mivujo inayopelekea upotevu wa huduma hiyo.

**Vile vile,** kadhiya ya umeme mdogo na ukatikaji wa mara kwa mara wa huduma hiyo, nayo imekua ikishuhudiwa katika maeneo mengi. Kwa hakika ukosefu wa huduma hizi kunaiweka jamii katika wakati mgumu kwani na kuwapunguzia muda wa kushiriki katika harakani na mipango mingine ya kujiendeleza na kuinua hali zao za kiuchumi na kimaendeleo. Hivyo, Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara ijipange na isimamie vizuri na ihakikishe Vipaombele wanavyojiwekea wanavifikia na vinatoa matunda yaliyokusudiwa.

**Hali ya Maji Nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kupongeza jitihada za Wizara za kutatua changamoto zilizopo katika suala zima za upatikanaji wa maji safi na salama, bado taarifa za Wizara zinabainisha kwamba kuna mapungufu ya uzalishaji wa maji kwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kwa upande mwengine Kamati inashauri Kiwango cha maji kinachozalishwa kifuatiliwe na kidhibitiwe ili kuhakikisha maji hayo yanawafikia walengwa badala ya kupotea kutokana na mivujo na uchakavu wa miundombinu ya maji iliyopo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaunga mkono juhudi za Serikali kupitia Wizara hii katika kukabiliana na utatuzi wa changamoto ziliopo katika suala la upatikanaji wa Huduma ya maji safi na salama ikiwemo uimarishaji wa uzalishaji wa maji, mifumo ya usambazaji, pamoja na uunganishwaji wa maji kwa wananchi. Kamati inashauri juhudi hizo kubwa za Serikali ziende sambamba na matokeo mazuri na yenye tija katika upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika nyumba na mitaa yote ambayo ndio kiu kubwa ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imaihimiza Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Maji kuendelea kuisimamia Miradi Mikubwa sita ya maji iliyopo pamoja na kukamilisha taratibu za kuanza Miradi mipya iliyopangwa ili kuimarisha huduma za maji hapa nchini.

**Vile vile,** Kamati inashauri kuangaliwa suala la uvunaji wa maji machafu (Maji Taka) pamoja na maji ya mvua ili yaweze kutumika katika shughuli nyenginezo ikiwemo umwagiliaji na ukoshaji wa vyombo vya moto na kuacha maji safi yakatumika katika shughuli za matumizi ya kawaida ya kijamii.

## Mageuzi ya Uendeshaji na Usimamizi wa ZAWA

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati inaafiki uamuzi wa Serikali wa kushirikisha na wawekezaji binafsi (Kampuni ya Rand Water) kutoka Afrika ya Kusini. Kamati inaamini kuwa mageuzi haya yatakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi na Serikali ikiwemo;-

1) Kuimarika na kuharakisha utoaji wa huduma za maji kwa wananchi,
2) Kuongezeka kwa wigo wa matumizi ya Teknolojia na Mifumo ya kisasa,
3) Kuipunguzia mzigo Serikali katika uwekezaji wa baadhi ya miundombinu,
4) Kuondosha hali ya kuziendesha Taasisi zetu kimazoea,
5) Kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato,
6) Kuongeza imani kwa wananchi katika huduma ya maji.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, Kamati inatahadharisha kwamba pamoja na matarajio ya kuimarishwa kwa huduma za upatikanaji wa maji kupitia mwekezaji huyo, fursa hiyo isitumike vibaya kwa kuwakandamiza wafanyakazi na wananchi hasa wanyonge kwa kisingizio cha ufanisi wa ukusanyaji wa mapato.

## Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Umeme

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ina wasi wasi na hatima ya upatikanaji wa nishati ya umeme hapa Zanzibar. Wasiwasi huu unakuja kufuatia kuendelea kuyoyoma kwa Megawati, kulingana na uwezo wa waya zinazotumika hivi sasa kuleta umeme katika visiwa vyetu

vya Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya Changamoto hiyo ya kuzidiwa kwa waya zetu, Kamati ilichambua changamoto nyengine katika sekta hii ikiwemo uchakavu wa miundombinu ya umeme, kuzidiwa kwa baadhi ya njia za Umeme, kuongezeka kwa mahitaji ya umeme kutokana na kuunganishwa kwa wateja wapya na wawekezaji katika ukanda wa utalii. Pia, kumekua na kadhiya kubwa ya kukatika kwa umeme mara kwa mara kwa baadhi ya maeneo.

Kamati inakubaliana na mikakati ya Wizara ya kukabiliana na utatuzi wa changamoto hizo kama zinavyoonekana katika hotuba ya mheshimiwa Waziri.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaafiki uamuzi wa Serikali wa kuendelea kushirikiana na wawekezaji binafsi kwa baadhi ya maeneo ya uwekezaji katika upatikanaji wa huduma hii muhimu ya umeme kwa wananchi katika maeneo yao. Vile vile, Kamati inahimiza kuendelea na tafiti na michakato ili kubaini na kutafuta vianzio vyengine vya umeme ikiwemo umeme wa mawimbi ya Bahari na upepo na jua.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati ZURA**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilichambua utekelelezaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA), ambapo pamoja na mengine Mamlaka hiyo ilifanya ukaguzi wa miundombinu ya umeme katika kituo cha Ras Kiromoni, kinacholeta umeme katika kisiwa cha Unguja na Mnyanjani Tanga kinachopeleka umeme katika Kisiwa cha Pemba na

kuibua changamoto kadhaa katika vituo hivyo kama zilivyoorodheshwa katika hotuba ya Mhe Waziri. Kamati yetu ambayo nayo imeshafika katika vituo hivyo na kubaini changamoto hizo hizo inaendelea kuikumbusha Wizara kuzitatua kwa haraka ili zisiendelee kuleta athari katika maeneo hayo kwani ndio roho ya umeme katika visiwa vyetu.

Miongoni mwa maeneo yanayohitajika kufanyiwa marekebisho ni mmong'onyoko wa ardhi katika sehemu iliyoanza kulazwa waya kuelekea Fumba katika kituo cha Ras Kiromoni, ambapo Kituo cha Mnyanjani Tanga kinakabiliwa na ukosefu wa kamera za ulinzi, taa kwa ajili ya usalama pamoja na bango la tahadhari.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza juu ya utekelezaji wa malengo iliyojiwekea Mamlaka hapo mwakani ambayo ni kuimarisha nyenzo za udhibiti wa huduma za Maji na Nishati pamoja na kuimarisha uwezo wa Taasisi wa kudhibiti huduma za Maji na Nishati.

**Sekta ya Nishati**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini kwa udhibiti mzuri wa mchanga, usimamizi wa kielektroniki pamoja na adhabu kwa wanaokiuka utaratibu wa maliasili zisizorejesheka suala ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa ukusanyaji wa mapato ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na pongezi hizo bado Wizara inakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa mchanga na rasilimali nyengine zisizorejesheka. Hili tumelibaini baada ya Kamati kutembelea maeneo ya uvunaji huko Donge na kujiridhisha kuwa kuna changamoto zifuatazo: -

a) Ufinyu wa ardhi ukilinganisha na mahitaji ya ujenzi yaliyopo,

b) Uchimbaji wa mchanga katika maeneo ya kilimo,

c) Uvunaji wa rasilimali katika maeneo yasiyo rasmi,

d) Usafirishaji wa rasilimali hizo katika njia zisizorasmi.

Kamati inaendelea kusisitiza kufuatiliwa na kufanyiwa kazi changamoto hizo kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

**Mheshimiwa Spika,** wakati tunajadili makadirio yanayohusu kusimamia huduma za upatikanaji wa Madini, Kamati ilihoji Mgao wa Matumizi wa asilimia 70 za Mapato yanayotokana na uchimbaji wa mchanga zinazokwenda Serikalini, na kubaini kuwa sehemu kubwa ya mapato hayo hurudi Wizarani. Kamati inashauri kuwa Sehemu ya mapato hayo yanayokwenda Wizarani yatumike katika kuyahuisha maeneo ya uvunaji badala ya jukumu hilo kupewa mmiliki wa eneo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati yetu, kwa mara nyengine napenda kukupongeza tena kwa uongozi wako pamoja na wasaidizi wako. Kwa hakika, busara na hekima zako zimeliwezesha Baraza letu kutekeleza vyema wajibu wake wa kuisimamia Serikali kwa ustadi wa hali ya juu. Kamati yetu inakuahidi ushirikiano wa hali ya juu na tunakuombea afya njema, maisha marefu pamoja na mafanikio katika safari zako za kisiasa.

Vile vile, tunamuomba Mwenyezi Mungu kutujaalia mafanikio mema sisi sote humu ndani ili tuendelee kuwatumikia wananchi wetu na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa ushirikiano wao mkubwa katika

utekelezaji wa majukumu ya Kamati, haswa wakati wa uchambuzi wa bajeti na hatimae kukamilisha taarifa hii. Kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa wajumbe hawa naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

| Nam | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Yahya Rashid Abdalla | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe.  Aza Januari Joseph | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ameir Abdallah Ameir | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Hassan Hamad Omar | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Simai Mohammed Said | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed | Mjumbe |
| 10. | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |
| 11. | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| 12. | Ndg. Saad Othman Saad | Katibu |

**Mheshimiwa Spika*,*** Pia napenda kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati tukijadili bajeti hii. Vile vile, nawashukuru watendaji wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia Makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mara nyengine tena napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha hotuba hii kwa niaba ya

Kamati, na pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuifatilia kwa ukaribu sana hotuba hii. Ni matumaini yangu kuwa Wajumbe wataichangia, wataijadili na hatimae kuipitisha Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** naunga Mkono Hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante,

**(Yahya Rashid Abdulla),**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**